MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Mbinu Zinazozua Mielekeo ya Wanafunzi katika Ufundishwaji wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Gatuzi Dogo la Masaba Kusini

Lena Nyandwaro[a] *, James Ontieri[a], Sangai Mohochi[b]

[a]*Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Rongo.*

[b]*Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii.*

**IKISIRI**

Ili mtaala wa elimu uweze kutekelezwa kwa njia inayofaa, ni muhimu kubaini mielekeo ya wadau husika. Hii ni kwa sababu mielekeo husaidia kujua mtazamo wao kuhusu mtaala huo, sababu za mielekeo yao na mikakati kuwekwa ili kuhakikisha mtaala unatekelezwa vilivyo. Walimu na wanafunzi ni baadhi ya wadau wanaohusika katika utelekezaji wa mtaala. Katika Mtaala wa Umilisi, Kiswahili ni somo la lazima linalofundishwa katika shule ya msingi. Ufundishaji wake unahusu wanafunzi kufanya mazoezi wakielekezwa na walimu, lengo likiwa ni kujenga umilisi wao katika lugha ya Kiswahili. Tafiti zimeonyesha kuwa walimu wana umuhimu kwa wanafunzi kwani hutagusana na wao sana shuleni. Inatarajiwa walimu wanaofundisha somo la Kiswahili watakuwa na athari chanya au hasi kwa mielekeo ya wanafunzi, suala ambalo makala haya yalitaka kubaini. Nadharia ya Kitendo Kinachofuata Mantiki ya Ajzen & Fishbein (1980) iliongoza makala haya. Data ilikusanywa kupitia ushuhudiaji miongoni mwa wanafunzi wa gredi ya tatu kutoka shule ishirini zilizoteuliwa kimaksudi katika gatuzi dogo la Masaba Kusini, kaunti ya Kisii. Ilibainika kuwa wanafunzi walikuwa na mielekeo chanya na hasi kuhusu Kiswahili kutegemea namna walivyofundishwa na walimu wao. Pia, kuna wanafunzi ambao walionyesha unasibu katika mielekeo yao. Makala haya ni muhimu kwani yatawasaidia walimu kufahamu athari yao kwa wanafunzi na kuboresha ufundishaji wao wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Mielekeo,
Mtaala wa Umilisi,
Ufundishaji,
Ufundishwaji.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 4 Juli 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 30 Octoba 2025
Tarehe ya Kukubalika: 02 Novemba 2025
Mtandaoni: 28 Novemba 2025

## 1. Utangulizi

Ajzen & Fishbein (2020) wanaeleza kuwa mielekeo ni namna mtu anavyotathmini dhana au hali fulani kwa njia chanya au hasi. Hiki ni kile anachoamini kuhusu matokeo ya kujihusisha na dhana, hali au kufanya kitu fulani. Ikiwa binadamu anaamini kitu kitakuwa na manufaa kwake, atakuwa na mielekeo chanya kukihusu na ikiwa anaamini hakitamfaa, atakuwa na mielekeo hasi kukihusu. Makala haya yalitalii mbinu zinazozua mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi.

Bataineh & Tasnimi (2014) wanaeleza kuwa ufundishaji wa lugha katika Mtaala wa Umilisi unahusu mwanafunzi kufundishwa lugha kwa kuzingatia mazingira yake halisi yaani mwalimu atoe mifano na vifaa vya ufundishaji katika mazingira anamokulia mwanafunzi. Pili, msisitizo huwekwa katika utendaji yaani mwanafunzi awe na uwezo wa kutumia maarifa aliyopewa kuhusu lugha badala ya kuweka maarifa hayo akilini. Tatu, ufundishaji wa lugha umegawanywa katika vijisehemu vidogovidogo ili mwanafunzi awe na uelewa wa kina kuhusu lugha husika. Mwisho, umilisi wa wanafunzi kuhusu lugha husika hupimwa kupitia utahini wa kila mara lengo likiwa ni mwalimu kubaini ikiwa mwanafunzi amefikia matarajio au la. Kulingana na KICD (2018), mwalimu anapofundisha Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi anapaswa kuweka mahitaji ya mtoto mbele na kumpa mwanafunzi mazoezi ili afikie kiwango cha juu cha umilisi. Kinachobainika ni kuwa katika Mtaala wa Umilisi, suala la utendaji ni la kimsingi. Suala hili la utendaji ni suala geni katika ufundishaji na ufundishwaji wa somo la Kiswahili na inatarajiwa kwamba wanafunzi watakuwa na mielekeo tofauti kulihusu kutegemea wanavyoelekezwa na kufundishwa na walimu wao. Ajzen & Fishbein (2020) wanaeleza kuwa binadamu huwa na mielekeo tofauti kuhusu hali ngeni.

Ufundishaji wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi unamtarajia mwalimu amwelekeze mwanafunzi kwa njia inayofaa ili afikie kiwango cha juu cha umilisi katika somo la Kiswahili. Katika mchakato wa kuelekeza na

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: nyandwarolena@gmail.com

Mhariri: Leonard Mwita, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.

Nukuu: Nyandwaro L., Ontieri J., & Mohochi S. (2025). Mbinu Zinazozua Mielekeo ya Wanafunzi katika Ufundishwaji wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Gatuzi Dogo la Masaba Kusini. Jarida la Kiswahili Sanifu 2(2), 19 – 25. https://doi.org/10.61889/jakisa.v2i2.119.

© 2025 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

kuwafundisha wanafunzi, inatarajiwa kuwa mwalimu atakuwa na athari ya moja kwa moja katika mielekeo ya wanafunzi kuhusu wanavyofundishwa. Kulingana na Yadav na Baniata (2013), mwalimu huathiri mwanafunzi kwa njia moja au nyingine kwa sababu ndiye anamfundisha na hutangamana naye kila mara. Isitoshe, Ulug na wenzake (2011) wanaeleza kuwa wanafunzi huiga yale wanayoambiwa au yanayofanywa na walimu wao kwa sababu wanatagusana na kutangamana na wao kila mara. Kwa hivyo, inatarajiwa kuwa walimu wanaofundisha Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi watakuwa na athari chanya au hasi kwa wanafunzi wao, jambo linalotafitiwa katika makala haya. Pia, wanasema kwamba athari ya walimu kwa wanafunzi huvuka mipaka ya wakati na huathiri takriban maisha yao yote. Kauli hii ilijitokeza katika utafiti wa Kahveci (2023) ambapo alibaini kuwa wasailiwa wake ambao walikuwa wanafunzi wa vyuo vikuu walisema kuwa waliathiriwa kimielekeo na walimu waliowafundisha katika shule ya msingi na upili. Matokeo ya utafiti wao yanashadidia umuhimu wa makala haya ambayo yalitaka kubaini mielekeo ya wanafunzi kuhusu namna wanavyofundishwa Kiswahili na walimu wao kwa sabau athari yao huwa kwa muda mrefu katika maisha ya mwanafunzi.

Kulingana na Codina na wenzake (2018), namna mwalimu anavyofundisha, umahiri wake katika somo analofundisha, anavyopanga kazi yake na jinsi anavyowapa wanafunzi motisha huathiri mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo husika. Pia, Fehintola (2014) anasema kuwa mwalimu anapaswa kuwa na mielekeo chanya anapofundisha lugha ili awaathiri wanafunzi wake kwa njia chanya. Anaeleza kuwa uchanya wa mwalimu anapofundisha hujitokeza kupitia anavyopanga somo lake darasani, mbinu anazoziteua na kuzingatia anapofundisha na jinsi anavyowasiliana na wanafunzi wake anapofundisha. Ili mwalimu anayefundisha Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi awe na athari faafu kwa wanafunzi wake, anatarajiwa kuchagua mbinu bunifu na changamfu anapofundisha, apange kazi yake kwa njia inayofaa na ambayo wanafunzi wataelewa kwa haraka. Okiya na wengine (2025), wakichunguza viwango vya makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi wanadokeza kuwa mbinu za ufundishaji ni miongozi mwa mambo yanayoathiri ufundishaji wa Kiswahili na kuathiri mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiswahili. Matumizi ya mbinu zisizofaa huathiri uelewa wa wanafunzi na kusababisha makosa ya kisarufi katika viwango vyote vya lugha. Wanapendekeza matumizi ya mbinu faafu za kufundisha na uimarishwaji wa mikakati ya kufundisha somo la Kiswahili.

Liu na wenzake (2017) wanasema kuwa mielekeo chanya wa walimu kuhusu masomo wanayofundisha darasani huchangia katika kujenga mazingira mazuri ya ufundishaji darasani. Pia, hukuza mawasiliano yanayofaa miongoni mwa wanafunzi hasa wanapowasiliana kwa kutumia lugha wanayofundishwa. Kwa upande mwingine, wanaeleza kuwa mielekeo hasi husababisha ukosefu wa mawasiliano kati ya walimu na wanafunzi wanapofundishwa lugha husika. Ili ufundishaji wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi ukamilike na malengo yake kuafikiwa, kutokana na maelezo ya watafiti hawa, pana haja ya kutathmini ikiwa mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufundishwaji wa Kiswahili inaathiriwa na walimu kwa njia chanya au hasi. Lippert (2017) anaeleza kuwa sio rahisi mwalimu mwenyewe kutathmini athari yake kwa wanafunzi anapofundisha kwa sababu anaweza kuwa na mapendeleo. Anapendekeza, wanafunzi wanaofundishwa na walimu husika wanaweza kuhojiwa au tabia yao kushuhudiwa ili kubaini wanavyoathiriwa na walimu wao. Katika makala haya, tabia ya wanafunzi ilishuhudiwa walipokuwa wanafundishwa somo la Kiswahili.

## 2. Nadharia ya Utafiti

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Kitendo Kinachofuata Mantiki iliyoasisiwa na Ajzen & Fishbein (1980). Kulingana na nadharia hii, mielekeo hutumiwa kutathmini matendo ya binadamu na huathiriana kimielekeo katika mazingira yake. Pia, binadamu huchukuliwa kama kiumbe aliye na uwezo wa kutumia maarifa aliyopata kwa utaratibu na kufanya uamuzi wake kwa sababu ni kiumbe aliye na urazini. Nadharia hii inaeleza kuwa binadamu akiwa na mielekeo chanya kuhusu hali au kauli fulani atafurahia kufanya na kuendeleza kauli hiyo na ikiwa ana mielekeo hasi, basi hatakuwa na furaha kutekeleza hali au kauli hiyo. Makala haya yalitaka kutathmini ikiwa mielekeo ya wanafunzi iliathiriwa na namna walimu waliwafundisha Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi.

Ajzen & Fishbein (2020) wanaeleza kuwa licha ya kuwepo kwa uwezekano wa binadamu kuathiriana kimielekeo, wakati mwingine kwa sababu ni kiumbe aliye na urazini, anaweza kukosa kuathiriwa na wenzake, yaani, mielekeo huwa ni nasibu. Kwa hivyo, makala haya pia yalitaka kubaini ikiwa wanafunzi walionyesha mielekeo chanya au hasi kuhusu Kiswahili bila kuathiriwa na walimu wao. Kulingana na nadharia hii, uchanya na uhasi hupimwa kutokana na majibu ya wasailiwa kuhusu kauli walizoulizwa au zilizoshuhudiwa. Katika utafiti huu, tabia chanya ambayo wanafunzi walionyesha na kushuhudiwa na mtafiti wakati walimu walipowafundisha Kiswahili ilichukuliwa kuwa wanafunzi waliathiriwa kwa njia chanya na walimu. Kwa upande mwingine, tabia hasi ambayo wanafunzi walionyesha iliashiria athari hasi kutoka kwa walimu walipowafundisha Kiswahili.

## 3. Mbinu za Utafiti

Muundo wa utafiti ulikuwa elezi. Creswell (2009) anaeleza kuwa muundo elezi unahusu kukusanya data nyanjani kisha data hiyo huchanganuliwa kwa kutolea maelezo. Eneo la utafiti lilikuwa gatuzi dogo la Masaba Kusini lililo katika Kaunti ya Kisii. Wasailiwa walikuwa wanafunzi wa gredi ya tatu kutoka shule ishirini zilizoteuliwa kimaksudi. Idadi ya wanafunzi darasani ilikuwa takriban wanafunzi 60 hadi 70 katika kila gredi ya tatu iliyoshuhudiwa katika shule hizo ishirini. Makala haya yalijikita katika wanafunzi wa gredi ya tatu kwa sababu wamepevuka kimawazo ikilinganishwa na wanafunzi wa gredi ya kwanza na pili. Ikumbukwe kwamba ni katika gredi ya kwanza hadi tatu ambapo ufundishaji wa Kiswahili unahusisha kufanya mazoezi ya Kiswahili kwa wingi, jambo ambalo ni geni kwani halipo

katika Mtaala wa 8-4-4. Data ilikusanywa kupitia ushuhudiaji wa tabia yao walipofundishwa Kiswahili, walivyojibu maswali darasani katika somo la Kiswahili na lugha waliyotumia kuwasiliana na walimu na wanafunzi wenzao. Oladipo na wenzake (2015) wanaeleza kuwa ushuhudiaji unahusu mtafiti kutazama matendo ya wasailiwa nyanjani. Jumla ya kauli nne zilishuhudiwa ili kubaini ikiwa walimu walikuwa na athari kwa mielekeo ya wanafunzi kuhusu walivyofundishwa Kiswahili. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo.

## 4. Uhusiano wa Mbinu za Ufundishaji na Mielekeo ya Wanafunzi katika Ufundishwaji wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi

Jinsi mwalimu anavyofundisha darasani, matayarisho yake na mbinu anazochagua na kuteua anapofundisha huwa na athari chanya au hasi kwa wanafunzi (Kahveci, 2023). Katika kazi hii, mielekeo ya wasailiwa kuhusu kauli hii ilitarajiwa kujitokeza kupitia walivyoitikia somo la Kiswahili wakifundishwa na walimu wao.

### 4.1. Walimu Wanavyowafundisha Kiswahili

Kupitia ushuhudiaji, ilibainika kuwa asilimia 45 ya walimu waliwafundisha wanafunzi kwa pupa na ukali. Hii iliwafanya baadhi ya wanafunzi kuwa na uoga darasani, hali ambayo ilichochea mielekeo hasi miongoni mwa asilimia 32 ya wanafunzi walioshuhudiwa. Wanafunzi hawa walionekana kuogopa kujibu maswali na mazoezi ambayo walipewa darasani baada ya kufundishwa mada mbalimbali za Kiswahili. Pryror & Johnson (2018) wanaeleza kuwa walimu ambao hufundisha wanafunzi kwa njia ya ukali ni ishara kuwa wana mielekeo hasi kuhusu somo wanalolifundisha. Ukali huu huathiri wanafunzi kwa njia hasi na matokeo yake ni wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu somo hilo. Hali hii huchangia utendaji duni wa mazoezi na huwa na athari hasi katika umilisi wao. Puhakka na wenzake (2021) wanasema kuwa walimu kufundisha kwa ukali kunaweza kusababishwa na hali kama vile dhuluma za kisaikolojia na uchovu wa kufanya kazi nyingi. Kwa hivyo, pana haja ya mwalimu kujaribu kuweka kando sababu hizo ili afundishe kwa njia isiyo ya ukali huku akikumbuka kuwa anawaathiri wanafunzi kwa kiwango kikubwa.

Ajzen & Fishbein (2020) wanaeleza kuwa wakati mwingine, binadamu wanaweza kutoathiriana kimielekeo yaani mielekeo ni nasibu. Hali hii ilijitokeza miongoni mwa asilimia 41 ya wanafunzi ambao kupitia ushuhudiaji, walionekana kutokuwa makini walimu walipofundisha Kiswahili darasani. Walimu waliokumbana na changamoto hii walionekana kujaribu kudhibiti tabia ya wanafunzi kwa kuwaelekeza namna walipaswa kuwa darasani na kushiriki wanapofundishwa. Walimu hawa waliweza kudhibiti tabia ya wanafunzi kwa kuwateua kimaksudi wajibu maswali darasani. Waliojibu sahihi kupitia maelekezo ya mwalimu darasani walipigiwa makofi na wanafunzi wengine kama njia ya kuwatuza kwa kuonyesha tabia inayofaa. Pia, walimu walitumia mamlaka yao kuwaamuru wanafunzi wawe makini na kuwaahidi tuzo ikiwa watatulia na kuwa makini wanapofundishwa Kiswahili. Hali hii ya walimu kuwaelekeza wanafunzi kwa njia inayofaa iliashiria mielekeo chanya kutoka kwa walimu. Wanafunzi darasani walionekana kusikiliza kwa utiifu na utulivu walivyoelekezwa na walimu wao, hali iliyoashiria athari chanya kutoka kwa walimu. Olubukola (2018) anasema kuwa walimu walio na mielekeo chanya wana uwezo wa kudhibiti tabia ya wanafunzi darasani na kuwaelekeza kwa njia inayofaa wanapowafundisha darasani.

Kwa upande mwingine, asilimia 55 ya walimu walipokuwa wanafundisha walionekana kuwahimiza wanafunzi kulipenda somo la Kiswahili. Kupitia ushuhudiaji, ilidhihirika kuwa wanafunzi hawa waliotiwa moyo walijaribu kujibu maswali waliyoulizwa darasani, walijituma kufanya mazoezi ya Kiswahili kwa njia sahihi na waliitikia somo kwa njia chanya. Walimu waliwahongera wanafunzi hawa kwa njia ya mdomo na kuwalekeza wanafunzi kupigiana makofi walipofanya mazoezi kwa njia sahihi. Hali hii iliashiria mielekeo chanya miongoni mwa wanafunzi ambao walikuwa wameathiriwa kwa njia chanya na walimu wao. Ajzen & Fishbein (1980) wanaeleza kuwa binadamu anapokuwa na mielekeo chanya kuhusu kauli fulani, hufurahia kutekeleza kauli hiyo. Katika utafiti huu, mielekeo chanya ilidhihirika miongoni mwa walimu kupitia njia changamfu walizoteua ya kufundisha na kuhusisha wanafunzi walipofuwafundisha somo la Kiswahili darasani.

Pia, walimu hawa waliwafundisha na kuwaelekeza wanafunzi kwa njia sahili, bunifu na inayoeleweka hasa walipowafundisha msamiati wa Kiswahili. Darasani, mtafiti alishuhudia majedwali na michoro ya kufundisha mada mbalimbali za Kiswahili. Leoanak & Amalo (2018) wanasema kuwa walimu walio na mielekeo chanya kuhusu ufundishaji wa lugha hupenda kutumia mbinu za ufundishaji zilizo bunifu, sahili na changamfu ili kuwachangamsha wanafunzi darasani na kuwafanya wapende lugha husika. Katika utafiti huu, mbinu bunifu ambazo walimu waliteua ziliwafanya wanafunzi kushiriki kikamilifu wakati walifundishwa, hali iliyodhihirisha mielekeo chanya kwa walimu kuhusu Kiswahili. Mielekeo chanya miongoni wanafunzi kuhusu namna walivyofundishwa ilidhihirika kupitia uchangamfu wao darasani na jinsi walivyoshiriki kikamilifu wakati wa somo la Kiswahili. Walisoma maneno ubaoni na kwenye chati kwa kutumia Kiswahili sanifu kama walivyoelekezwa na matamshi yao wa maneno yalikuwa mazuri. Hali hii ilionyesha kuwa wanafunzi walielewa na kupenda somo la Kiswahili, hali iliyochangiwa na mbinu ambazo walimu wao walitumia kufundishia kwani zilikuwa sahili, changamfu na bunifu. Baada ya somo, mwalimu aliwauliza wanafunzi wakati wa mapumziko ikiwa walifurahia somo la Kiswahili na asilimia 68 ya wanafunzi walisema kuwa walipenda namna walimu wao waliwafundisha kwa kutumia michoro, picha na majedwali. Ajzen & Fishbein (1980) wanaeleza kuwa mielekeo huathiriana. Katika utafiti huu, ilibainika kuwa walimu walio na mielekeo chanya kuhusu somo la Kiswahili walichagua mbinu bunifu na changamfu za kufundishia wanafunzi, hali iliyowaathiri wanafunzi hao kwa njia kubalifu.

### 4.2. Mazoezi Wanayopewa katika Somo la Kiswahili

Mtaala wa Umilisi unasisitiza kuwa wanafunzi wapewe mazoezi baada ya kufundishwa. Mazoezi haya huwasaidia wanafunzi kutumia maarifa waliyopata darasani kiutendaji. Pia, husaidia walimu kupima umilisi wa wanafunzi wao kuhusu waliyofundishwa ili kubaini ikiwa wameelewa vipengele walivyowafudisha darasani au la.

Katika utafiti huu kupitia ushuhudiaji, ilibainika kuwa baadhi ya mazoezi ambayo wanafunzi walipewa yalikuwa magumu. Asilimia 34 ya wanafunzi walishindwa kufanya mazoezi hayo. Pia, asilimia 38 ya walimu walishuhudiwa kutowaelekeza wanafunzi namna ya kufanya mazoezi na kuwarekebisha kufanya marudio. Sababu ilikuwa idadi kubwa ya wanafunzi darasani. Katika shule zilizoshuhudiwa, wanafunzi walikuwa zaidi ya sitini darasani ilhali ni mwalimu mmoja aliyewafundisha na kuwaelekeza katika somo la Kiswahili. Idadi kubwa ya wanafunzi ni kinyume na mapendekezo ya kikosi cha rais kilichoteuliwa kushughulikia mabadiliko ya mtaala wa elimu nchini PWPER (2023) kilichopendekeza kuwa mwalimu mmoja anapaswa kushughulikia wanafunzi arobaini. Hali hii ilichangia walimu kuwapa wanafunzi mazoezi na kusahihisha vitabu vichache tu mwishoni mwa kipindi.

Wanafunzi hawa walionyesha kutokuwa makini kufanya mazoezi, hali iliyoashiria mielekeo hasi kuhusu mazoezi hayo ya Kiswahili. Hali hii ilichangiwa na wanafunzi kutoelekezwa kwa njia inayofaa na walimu wao. Liu & Jackson (2019) wanasema kuwa walimu wasiowasaidia wanafunzi kufanya marudio wala kuwapa maelekezo yanayofaa wanapotekeleza mazoezi wanayofanya huwa ni ishara ya kuwa mielekeo hasi kuhusu somo hilo. Hali hii kutoka kwa walimu itakuwa na athari hasi kwa wanafunzi kwa sababu wanafunzi hao hawatakuwa makini kufanya mazoezi waliyopewa. Erdogdu (2013) anaeleza kuwa mielekeo ya walimu na tabia yao huathiri kwa kiasi kikubwa namna wanafunzi watafanya mazoezi na matokeo ya mazoezi hayo.

Kati ya shule ishirini zilizoshuhudiwa katika utafiti huu, asilimia 98 hazikuwa na mtandao wala vifaa vya kidijitali vya kufundishia Kiswahili. Katika baadhi ya shule hizo, wanafunzi watatu au wanne walitumia kitabu kimoja cha kozi ya Kiswahili kusoma na kufanya mazoezi darasani. Ukosefu wa vitabu, mtandao na vifaa vingine vya kufanikisha wanafunzi kufanya mazoezi ya Kiswahili uliwafanya baadhi ya walimu kutowapa wanafunzi mazoezi ya kufanya darasani na nyumbani. Hali hii ilichangia walimu kuwa na mielekeo hasi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili kwa sababu walishindwa kupima umilisi wa wanafunzi kikamilifu kupitia mazoezi. Sugano & Mamolo (2021) wanaeleza kuwa ukosefu wa vifaa vya kufundishia lugha hulemaza ufundishaji, hali inayochangia mielekeo hasi miongoni mwa walimu wanapofundisha. Katika utafiti huu, hali hii iliathiri wanafunzi kwa njia hasi kwa sababu hawakuweza kufanya mazoezi ambayo ni kipimo cha uelewa wao katika somo la Kiswahili. Wanafunzi kufanya mazoezi ni njia mojawapo ya kuweka maarifa waliyopata darasani kiutendaji.

Licha ya uhaba wa vitabu na vifaa mbalimbali vya kufundishia Kiswahili, asilimia 66 ya wanafunzi walionyesha mielekeo chanya kuhusu kauli hii ambayo ilidhihirika kupitia uitikiaji chanya na uchangamfu waliodhihirisha walipofanya mazoezi darasani. Asilimia 62 ya walimu wao waliwaelekeza vilivyo walipofanya mazoezi, walisahihisha na kuwarejeshea vitabu vyao. Mazoezi wanayofanya wanafunzi husaidia kukuza na kuboresha sarufi yao katika somo la Kiswahili. Ulum (2020) anasema kuwa walimu huelekezwa kuwapa wanafunzi mazoezi ili wawe na uwezo wa kuhifadhi akilini waliyofundishwa darasani. Kwa hivyo baada ya kuwapa wanafunzi mazoezi, walimu wanatarajiwa kusahihisha na kuwaelekeza wanafunzi kwa njia inayofaa. Lengo ni kuwarekebisha wanapokuwa wamepotoka wakifanya mazoezi ili kukuza umahiri wao katika Kiswahili. Utoaji wa mazoezi haya hulingana na maelekezo ambayo wamepewa kwenye silabasi, vitabu vya kozi na maazimio ya kazi waliyotayarisha. Koskal (2008) anasema kuwa walimu wana jukumu la kuwaelekeza wanafunzi kwa njia inayofaa kwa kuwapa maswali na mazoezi ili kuwasaidia kujenga umilisi wao katika masomo husika. Sturgis (2015) anaeleza kuwa ni jukumu la walimu kuwapa wanafunzi wao msaada wa kutosha wanapotekeleza mazoezi mbalimbali darasani ili wawe na umilisi unaofaa katika masomo husika.

Kulingana na kauli hii, ni wazi kuwa walimu waliathiri mielekeo ya wanafunzi ya kufanya mazoezi ya Kiswahili. Ajzen & Fishbein (1980) katika Nadharia ya Kitendo Kinachofuata Mantiki, wanaeleza kuwa mielekeo huathiriana. Hali hii ilibainika pale ambapo walimu waliowapa wanafunzi mazoezi na kufuatilia waliwapa wanafunzi motisha ya kufanya mazoezi hayo na kuwafanya wawe na mielekeo chanya kinyume na wale ambao hawakufuatilia wanafunzi kufanya mazoezi. Pia, katika utafiti huu ilibainika kuwa ukosefu wa malighafi muhimu ya ufundishaji iliathiri mielekeo ya walimu kwa njia hasi walipofundisha Kiswahili na kuathiri wanafunzi.

### 4.3. Kuwasiliana na Wanafunzi Wenzao na Walimu kupitia Lugha ya Kiswahili

Kulingana na KICD (2018), mwanafunzi anapaswa kutumia maarifa aliyopokea darasani katika maisha yake ya kila siku. Njia mojawapo ya kuonyesha utendaji wa somo la Kiswahili ni wanafunzi kutumia Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku.

Katika shule kumi za umma zilizoshuhudiwa, ilibainika kuwa asilimia 74 ya wanafunzi walichanganya Kiswahili na lugha ya kiasili walipowasiliana na wenzao wakicheza uwanjani. Kwa upande mwingine, shule kumi za kibinafsi zilizoshuhudiwa, asilimia 67 ya wanafunzi walitumia Kiingereza walipowasiliana na wenzao wakicheza uwanjani.

Pia, ilishuhudiwa kwamba asilimia 46 ya walimu hawakuwa makini kutumia Kiswahili sanifu walipowasiliana na wanafunzi wao. Walimu hawa walichanganya lugha ya Kiswahili, kiasili na Kiingereza.

Kutokana na hali hii, ilidhihirika kuwa mawasiliano yaliendelezwa kwa kuchanganya lugha hizi tatu. Kwa hivyo, hali hii ya walimu kutokuwa makini kutumia Kiswahili pekee katika mawasiliano yao iliwafanya wanafunzi kutokuwa makini kutumia Kiswahili walipokuwa wakiwasiliana na wenzao. Walimu ambao walichanganya lugha wakiwasiliana na wanafunzi walifahamu sera ya shule kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza ila walikiuka sera hiyo. Walihisi kuwa ni muhimu kuchanganya lugha walipowasiliana na wanafunzi ili kupitisha ujumbe kikamilifu kwa wanafunzi. Katika utafiti wa Ulug na wenzake (2011), walibaini kuwa wanafunzi huiga tabia za walimu wao kwa sababu wana ukuruba na wao sana. Katika utafiti huu, hali hii ilidhihirika miongoni mwa wanafunzi ambao walichanganya lugha walipowasiliana kama vile walimu wao.

Kwa upande mwingine, asilimia 54 ya walimu walionekana kuwasiliana na wanafunzi wao katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hao walionekana kujaribu kutumia Kiswahili walipowasiliana na walimu pamoja na wanafunzi wenzao. Walimu walionekana kuwahimiza wanafunzi kukitumia Kiswahili, hali ambayo wanafunzi walizingatia. Hali hii iliwasaidia wanafunzi kuboresha matamshi yao na kutumia msamiati waliofundishwa darasani. Pia, walitumia Kiswahili kuwasiliana na wenzao kwa sababu ilikuwa ni sheria shuleni kuwa kila mwanafunzi alitarajiwa kuwasiliana na wenzake katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza na wengi walipendelea Kiswahili hasa katika shule za umma. Ajzen & Fishbein (2020) wanaeleza kwamba binadamu anaweza kuwa hana nia ya kutaka kufanya jambo ila kutokana na sheria au vizingiti alivyowekewa katika mazingira yake, akajipata akifanya na kupitia ufanyaji huo, akawa na mielekeo chanya au hasi kuhusu analotenda.

Katiba ya Kenya (2010) inaeleza kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Pia, Kiswahili kinatambuliwa kama Lingua Franka ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo, pana haja ya wanafunzi kuwa na umilisi wa kukitumia katika mawasiliano yao. Ili wanafunzi wawe na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali, walimu wao wanapaswa kuwa na mielekeo chanya kukihusu. Mielekeo chanya miongoni mwa walimu kuhusu Kiswahili yaweza kudhihirika kupitia namna wanavyokitumia wanapowasiliana na walimu wenzao, wanafunzi, kuwatuza wanafunzi wanaotumia Kiswahili wanapowasiliana na kuwahimiza wanafunzi kukitumia katika mawasiliano yao.

Walimu waliotumia Kiswahili kuwasiliana walionekana kuwapa wanafunzi motisha na ujasiri wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao. Hali hii ilidhihirika miongoni mwa asilimia 26 ya wanafunzi katika shule za umma na asilimia 33 ya wanafunzi katika shule za kibinafsi. Walimu hawa waliwatuza wanafunzi ambao walijaribu kuwasiliana kwa Kiswahili sanifu kwa kuwapa pipi, au kuwahongera kwa maneno chanya. Walimu walitumia maneno kama vile "kazi nzuri mwanafunzi kwa kuwasiliana kwa Kiswahili" na "heko kwa kuzingatia maneno sanifu katika mawasiliano yako nami na wanafunzi wenzako". Pia wanafunzi walituzwa vitabu vya hadithi vya Kiswahili, pipi na beji ya kuonyesha mwanafunzi bora wa Kiswahili. Oslon & Kendrick (2008) wanaeleza kuwa binadamu anapotuzwa kwa njia yoyote ile, iwe chanya au hasi, huwa na athari kwa matendo yake, hali iliyodhihirika katika kauli hii.

### 4.4. Kueleza, Kuelewa na Kutatua Masuala Mtambuko katika Lugha ya Kiswahili

Masuala mtambuko ni masuala ambayo yanaathiri binadamu katika mazingira yake kwa njia chanya au hasi. Kulingana na KICD (2018), haya ni masuala ambayo binadamu anapaswa kujifundisha kuishi na kukabiliana nayo katika maisha yake. Kwa hivyo, ni muhimu wanafunzi wafundishwe na kuelimishwa jinsi ya kukabiliana na masuala haya katika maisha yao ili wawe na maisha bora na uhusiano unaofaa na wanajamii wengine. Mtaala wa Umilisi unasisitiza umuhimu wa kufundisha masuala haya ili kumtayarisha mwanafunzi kukabiliana nayo kwa njia inayofaa. Masuala haya hufundishwa kupitia hadithi ambazo wanafunzi wanasoma, kusikiliza na mazoezi ya sarufi wanayofanya darasani. Katika Mtaala wa Umilisi, ufundishaji wa masuala mtambuko umejumuishwa katika kila mada ya Kiswahili kwa kuzingatia stadi za kusikiliza na kuzungumza, kuandika, kusoma na matumizi ya lugha.

Kupitia ushuhudiaji, asilimia 90 ya walimu walionyesha umahiri wa kufundisha masuala mtambuko kwa wanafunzi. Waliwafundisha kwa njia sahili na bunifu huku wakitoa mifano inayoeleweka kutoka kwa mazingira ya kawaida ya wanafunzi. Wanafunzi walionekana kupenda namna walivyofundishwa kwani walikuwa tayari kujibu maswali waliyoulizwa na kuonyesha jitihada katika kufanya mazoezi yaliyohusisha masuala mtambuko. Walimu walitumia michoro, vibonzo na picha mbalimbali kutoka kwenye mtandao walipofundisha masuala haya. Hali hii ilifanya ufundishaji wa masuala mtambuko kufana kutokana na namna wanafunzi walivyofurahia na kuchangamkia somo hilo. Walsh na wenzake (2020) wanaeleza kuwa mwalimu aliye na mielekeo chanya kuhusu somo analofundisha, hujaribu kupanga somo lake kwa njia inayoeleweka, hutumia mbinu za ufundishaji bunifu na sahili, hali ambayo huwa na athari chanya kwa wanafunzi. Hali hii ilijitokeza katika utafiti huu kwani uelewa na kujaribu kutatua masuala mtambuko kwa kutumia lugha ya Kiswahili kulionyesha mielekeo chanya miongoni mwa wanafunzi. Kwa jumla, wanafunzi walionyesha mielekeo chanya kuhusu kauli hii hali iliyoashirisha kuwa walimu waliwaathiri kwa njia chanya.

## 5. Hitimisho

Makala haya yamebaini kuwa wanafunzi walionyesha mielekeo chanya na hasi kuhusu somo la Kiswahili kutegemea namna walivyofundishwa na walimu wao. Hali hii inaonyesha kuwa mazingira (binadamu akiwemo) huathiri pakubwa mielekeo ya mtu kuhusu hali, dhana au kauli fulani. Kwa hivyo, pana haja ya walimu kujaribu kutumia mbinu zitakazokuza mielekeo chanya kuhusu ufundishaji wa Kiswahili ili kuathiri wanafunzi kwa njia chanya, hali ambayo itasaidia utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi kikamilifu. Makala haya yanapendekeza kuwa walimu watumie njia bunifu na changamfu za kufundisha

na kufanya mazoezi ya Kiswahili ili mwanafunzi afikie umilisi wa juu katika lugha ya Kiswahili.

## Marejeleo


Ajzen, I.,&Fishbein, M. (1980). *Understanding attitudes and predicting social behaviour*. Englewood, New Jersey, USA: Prentice Inc.

Ajzen, I., & Fishbein, M. (2020). Understanding attitudes and predicting social behaviour. Eaglewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall.

Bataineh, K.B. & Tasnimi, M. (2014), Competence based language teaching. Katika Express, an International *Journal of Multidisciplinary Research*. Juz 1(7).

Codina, N., Valenzuela, R., Pestana, J. V., & Gonzalez-Conde, J. (2018). Relations between student procrastination and teaching styles: Autonomy, supportive and controlling. *Psychology*. 9, 809. https://doi.org/ 10.3389/fpsyg.2018.00809.

Creswell, J. (2009). Research design: Qualitative, quantitative and mixed methods approach (Third edition). London: Sage Publications.

Erdogdu, M. (2013). Relationship between parental attitudes and teacher behaviour and students. *Journal of Education Faculty*. Vol. 14. Uk. 33-46.

Fehintola, J. (2014). Teachers' characteristics as correlates of students' academic performance among secondary school students in Saki West local government area of Oyo state. *Journal of Educational and Social Research*. Juz. 4 (6).

Fraser, L.E. (2014). Teacher Efficacy Beliefs: how general teachers feel towards English language learners. *Capstones paper* 828. Uk. 1-56.

Granados, F.C., Ramos, J.R., Guerrero, M.F., Redondo, F.M., Gordillo, M.A.G., Polero, P.& Adsuar, J.C. (2020). A descriptive study on the training and attitude of future teachers towards educational inclusion. *Sustainability*. Juz. 12 (19). Uk.1-14.

Hamer, L. & Keefe, R. (2013). Achieving change in students' attitude towards group projects by teaching group skills. *Journal of higher education theory and practice*. Uk. 25-33. https://via.library.depaul.edu/buspubs/71.

Kahveci, H. (2023). The positive and negative effects of teacher attitudes and behaviors on students' progress. *Journal of Pedagogical Research*. Vol.7 (1).

KICD. (2018). Basic education curriculum framework: Nurturing every learner's potential. Nairobi: Kenya Institute of Curriculum Development.

Koskal, N. (2008). Assessment of generic competences of teaching profession by teacher, school directorand consultants from the Ministry of Education. Pamukkale University *Journal of Education*. Juz. 23 (23). Uk. 36-46.

Leoanak, S.P.P. & Amalo, B. (2018). Teachers' beliefs and perceptions of code switching in English as foreign language classroom. SHS Web of Conferences 42, 00034.

Lippert, L.B. (2017). How mainstream teacher attitudes affect English language learner student learning in the mainstream classroom. School of Education and Leadership Student Capstone Projects. Imepakuliwa kutoka https://digitalcommons.hamline.edu/hse_cp/119.

Liu, H., Lin, C.H. & Zhang, D. (2017). Pedagogical beliefs and attitudes towards information and communication technology: A survey of teachers of English as a foreign language in China. *Computer Assisted Language Learning*. Juz. 30 (8). Uk. 745 - 765. https://doi.org/10.1080/09588221.2017.1347572.

Liu, L., & Jackson, J. (2019). Building learner self belif in oral communique via remarks. *Journal of Language Teaching and Research*. 10(3). Uk. 647-660.

Okiya, E.; Miruka, F. & Kang'ahi, M. (2025). Viwango vya Makosa ya Kisarufi katika Insha za Wanafuzi wa Mtaala wa Umilisi. *Jarida la Kiswahili Sanifi*. Juzuu 2.1:004 https.journals@mmust.ac.ke.

Oladipo, R., Ikimari, L., Kiplang'at, J. & Barasa, L. (2015). General research methods: Nairobi: Oxford University Press.

Olubukola, J. (2018). Teachers' professional attitudes and students' academic performance in secondary schools in Ilorin Metropolis of Kwara State. In eJournal of Educational Policy.

Oslon, M. & Kendrick, R. (2008). Origins of attitudes. In Crano, D na Prislim, R. (eds) Attitude and attitude change. New York: Psychology Press.

Presidential Working Party on Education Reform (PWPER). (2023). *Report of the presidential working party on Education Reforms*. Government of Kenya.

Pryor, N. J., & Johnson, C.C. (2018). Assessing the impact of instructors' terrible mindset on pupil fulfilment. Teachers College Record. 120(10). Uk 1-40.

Puhakka, I.J., Nokelainen, P. & Pylvas, L. (2021). Learning or leaving? Individual and environmental factors related to job satisfaction and turnover intention. Vocat. *Learn*. Juz. 14. Uk. 481-510.

Sturgis, C. (2015). Implementing competence education in K-12 systems: Insights from local leaders. In https://filles.eric.ed.gov/fulltext/ED557750.pdf.

Sugano, S. G. C. & Mamolo, L. A. (2021). The effects of teaching methodologies on students' attitude and motivation. In Meta-analysis. *Int. J. Instr*.14, 827–846. https://doi.org/10.29333/iji.2021.14348a.

The Government of Kenya. (2010). The Constitution. Nairobi: Government Printers.

Ulug, M. Odzen, S.M. & Eryilmaz, A. (2011). S.M. Ozden, A. Eryilmaz. The effects of teachers' attitudes on students' personality and performance. Procedia-Social. *Behavioral Sciences*. Juz. Uk. 738-742.

Ulum, O.G. (2020). The use of assignments in education. *Base for Electronic Educational Sciences*. Juz. 1 (1).

Walsh, P., Owen, P. A. Mustafa, N. & Beech, R. (2020). Learning and teaching approaches promoting resilience in student nurses: An integrated review of the literature. *Nurse Educational Practice*. Juz. 45 (8). https://doi.org/10.1016/j.nepr.2020.102748.

Yadav, M., & Baniata, H. (2013). Factorizing demotivation, finding motivation: A constructive approach to quality enhancement. *Procedia- Social & Behaviour Sciences*. Juz. 70. Uk. 120–130. https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2013.01.047.